

**TANGAZO LA UUZAJI WA VIWANJA ENEO LA MNAZI WILAYA YA  
LUSHOTO**

TAREHE: 12/08/2020

Halmashauri ya wilaya ya Lushoto imepima viwanja 738 katika kata ya Mnazi vikiwa na matumizi mbalimbali

Eneo lililopimwa viwanja linahadhi ya Mji mdogo kwa mujibu wa Tangazo la Serikali (GN) Na 176 la Tarehe 09/08/96. Eneo lilopimwa viwanja lina miundo mbinu ya maji, umeme na barabara inayopitika na lipo umbali wa kilomita 7 kutoka hifadhi ya mbuga ya wanyama ya Mkomazi .


Halmashauri inawatangazia wanachi wote kuomba kununua viwanja hivyo kwa kuchukua fomu ya maombi katika Ofisi za kata ya Mnazi na Ofisi ya Ardhi ya Halmashauri iliyopo Lushoto Mjini kuanzia tarehe 13-08-2020 mpaka 27-08-2020.

**BEI YA VIWANJA NI KAMA IFUATAVYO;**


SN	MATUMIZI	IDADI	BEI KWA SQM
1	MAKAZI	535	1,000/=
2	MAKAZI NA BIASHARA	123	1,500/=
3	BIASHARA	11	2,000/=
4	VIWANDA	16	5,500/=
5	VIWANDA VIDOGO	07	3,000/=
6	MOTELI	01	7,000/=
7	HOTELI	01	KWA TENDA
8	MASHAMBA YA MJINI	03	1,000/=
9	VIWANJA VYA KUABUDIA	04	2,500/=
10	VITUO VYA MAFUTA	02	KWA TENDA

Mara utakapopata kiwanja, utatakiwa kulipia asilimia 20% ya gharama ya kiwanja na deni litakalobaki utatakiwa kulipa ndani ya siku 90, kuanzia tarehe ya kupata kiwanja hicho. Zingatia kuwa malipo ya fomu hayatarejeshwa. Aidha endapo utashindwa kulipia kiwanja ndani ya siku tisini (90), kiwanja hicho atauziwa mtu mwingine bila kurejeshewa fedha zako ulizokwishalipa. Gharama hizi hazijumuishi maandalizi ya hati na umilikishaji wa kiwanja.

Imetolewa na ;

  
AYUB OMARY

KAIMU MKURUGENZI MTENDAJI (W)  
HALMASHAURI YA LUSHOTO.

  
MKURUGENZI MTENDAJI (W)  
LUSHOTO